# KILIMO *Bulletin*

*Toleo Maalum: Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani 2026*

*Machi, 2026*



**“Nawatakia Wanawake na Wasichana wote wa Tanzania na Duniani maadhimisho mema ya Siku ya Wanawake Duniani,”**

Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan
**Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**





*www.kilimo.go.tz*





Mhe. Daniel Chongolo (Mb)
**Waziri wa Kilimo**

Katika kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani 2026, uwekezaji wa Wanawake ni nguzo muhimu katika mageuzi ya kilimo ambapo Serikali chini ya Uongozi mahiri wa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, I nahakikisha Wanawake wanapata fursa mbalimbali katika Sekta ya Kilimo ili waweze kuongeza kipato na kujitegemea kiuchumi.

Nikiwa Waziri mwenye dhamana ya kusimamia Sekta ya Kilimo, nitaendelea kuhakikisha dhamira ya Serikali ya kushirikiana na wadau mbalimbali inatekelezwa ili kuwawezesha Wanawake kushiriki kikamilifu katika shughuli za kilimo. Hii itawawezesha kuwa na uzalishaji unaowaletea tija endelevu kwa ustawi wa familia zao na maendeleo ya Taifa kwa ujumla.

Serikali inalenga kuongeza tija ya kilimo kupitia utekelezaji wa Agenda 10/30 kwa kuhakikisha Sekta ya Kilimo inachangia kwa asilimia 10 katika pato la Taifa hadi kufikia mwaka 2030. Wanawake wanapewa kipaumbele maalum ili washiriki kikamilifu katika mnyororo mzima wa thamani wa kilimo, kuanzia uzalishaji hadi biashara ya mazao. Hii ni hatua ya kuhakikisha usawa wa kijinsia na kupunguza umaskini vijijini.

Vilevile, kupitia Mpango Kabambe wa Mageuzi ya Kilimo 2050 (Agriculture Master Plan 2050), Serikali imeweka mkakati wa muda mrefu wa kuendeleza kilimo chenye tija, chenye kuhimili mabadiliko ya tabianchi, na chenye kujumuisha makundi yote ya jamii. Wanawake wanachukuliwa kama wadau wakuu wa mageuzi haya, kwa kuwa uwezeshaji wao ni msingi wa kujenga uchumi imara na endelevu. Mpango huu unalenga si tu kuongeza uzalishaji, bali pia kuimarisha usawa wa kijinsia na kujenga kizazi kinachojitegemea kiuchumi.

Hongereni sana na nawatakia maadhimisho mema ya Siku ya Wanawake Duniani 2026.



Mhe. David Silinde (Mb)
**Naibu Waziri wa Kilimo**

Ni muhimu kutambua kuwa Wanawake si washiriki tu wa Sekta ya Kilimo, bali pia ni viongozi wenye uwezo wa kuleta mabadiliko makubwa. Tunapaswa kuhakikisha Wanawake wanapewa nafasi za uongozi katika vyama vya ushirika, mashirika ya kilimo, na taasisi za mafunzo ya kilimo. Kupitia nafasi hizi, Wanawake wataweza kushiriki katika maamuzi makuu yanayohusu sera, uwekezaji, na usimamizi wa rasilimali.

Katika Sekta ya Kilimo, tumeendelea kuimarisha mifumo ya upatikanaji wa mikopo na mitaji kwa Wanawake wakulima na wafanyabiashara wa kilimo. Dhamira yetu ni kuwawezesha Wanawake kushiriki na pia kuongoza katika mnyororo wa thamani wa kilimo, kuanzia uzalishaji hadi masoko ya kimataifa.

Kwa kuweka Wanawake katika nafasi za uongozi, tunajenga Sekta ya Kilimo yenye usawa, inayojumuisha wote, na yenye uwezo wa kufanikisha malengo ya maendeleo endelevu. Wanawake viongozi katika kilimo watakuwa mfano wa kuigwa na watatoa dira ya mabadiliko kwa vizazi vijavyo.

Natoa wito kwa Watumishi Wanawake kuendelea kuwajibika katika kuunda mazingira wezeshi yatakayowawezesha wananchi kushiriki kikamilifu katika kilimo biashara, ili kufanikisha malengo ambayo Wizara imejiwekea ya kukuza kilimo kwa asilimia 10 ifikapo mwaka 2030.

Ni dhamira yetu kutafakari na kutafsiri kwa vitendo kauli mbiu ya mwaka huu isemayo: “Haki na Usawa kwa Wanawake na Wasichana: Msingi Jumuishi kufikia Dira 2050.” Kauli mbiu hii ni kielelezo cha kuimarisha mshikamano, usawa wa kijinsia, na uwezeshaji wa Wanawake katika safari ya kufikia maendeleo endelevu ya Taifa letu.

Hongereni sana na nawatakia maadhimisho mema ya Siku ya Wanawake Duniani 2026.



Bw. Gerald Mweli
**Katibu Mkuu**
**Wizara ya Kilimo**

Tunapoelekea Siku ya Wanawake Duniani 2026, nachukua nafasi hii kuwapongeza Wanawake kwa mchango wao mkubwa katika maendeleo ya Sekta ya Kilimo na ustawi wa jamii kwa ujumla.

Ni muhimu pia kutambua kuwa Wanawake si washiriki tu wa Sekta ya Kilimo, bali pia ni viongozi wenye uwezo wa kuleta mabadiliko makubwa. Tunapaswa kuhakikisha Wanawake wanapewa nafasi za uongozi katika vyama vya ushirika, mashirika ya kilimo, na taasisi za mafunzo ya kilimo. Kupitia nafasi hizi, Wanawake wataweza kushiriki katika maamuzi makuu yanayohusu sera, uwekezaji, na usimamizi wa rasilimali.

Katika Sekta ya Kilimo, tumeendelea kuimarisha mifumo ya upatikanaji wa mikopo na mitaji kwa Wanawake wakulima na wafanyabiashara wa kilimo. Dhamira yetu ni kuwawezesha Wanawake kushiriki na pia kuongoza katika mnyororo wa thamani wa kilimo, kuanzia uzalishaji hadi masoko ya kimataifa.

Natoa wito kwa Watumishi Wanawake kuendelea kuwajibika katika kuunda mazingira wezeshi yatakayowawezesha wananchi kushiriki kikamilifu katika kilimo biashara, ili kufanikisha malengo ambayo Wizara imejiwekea ya kukuza kilimo kwa asilimia 10 ifikapo mwaka 2030.

Ni dhamira yetu kutafakari na kutafsiri kwa vitendo kauli mbiu ya mwaka huu isemayo: “Haki na Usawa kwa Wanawake na Wasichana: Msingi Jumuishi kufikia Dira 2050.” Kauli mbiu hii ni kielelezo cha kuimarisha mshikamano, usawa wa kijinsia, na uwezeshaji wa Wanawake katika safari ya kufikia maendeleo endelevu ya Taifa letu.

Hongereni sana na nawatakia maadhimisho mema ya Siku ya Wanawake Duniani 2026.



Mha. Athumani J. Kilundumya
**Naibu Katibu Mkuu (Umwagiliaji na Zana za Kilimo)**

Uwezeshwaji wa kiuchumi kwa Wanawake kupitia upatikanaji wa rasilimali, mafunzo, teknolojia na mitaji ni nyenzo imara ya kuongeza tija na kipato katika kilimo, na hivyo kuchangia kwa kiasi kikubwa maendeleo endelevu ya kiuchumi nchini. Wanawake wanapopewa nafasi na msaada wa kutosha, wanaweza kuwa chachu ya mabadiliko makubwa katika Sekta ya Kilimo, hususan kwenye maeneo ya umwagiliaji na matumizi ya zana za kisasa za kilimo.

Ni kwa dhamira hiyo, Wizara itaendelea kushirikiana nanyi na kuhakikisha inaongeza wigo wa mazingira rafiki yatakayowawezesha kushiriki zaidi katika miradi ya umwagiliaji na upatikanaji wa zana bora za kilimo. Hatua hii inalenga kupunguza vikwazo vinavyowakwamisha Wanawake, ikiwemo ukosefu wa mitaji, elimu ya kiufundi, na teknolojia inayohitajika ili kuongeza uzalishaji.

Aidha, Wizara itahakikisha Wanawake wanapatiwa mafunzo ya kitaalamu kuhusu matumizi ya teknolojia za umwagiliaji na zana za kısasa za kilimo, ili waweze kutumia zana hizo kwa ufanisi na kuongeza mavuno. Mafunzo haya yatasaidia pia kupunguza utegemezi wa nguvu kazi ya mikono, na hivyo kuwapa nafasi ya kuendesha shughuli za kilimo kwa urahisi na kwa kiwango kikubwa zaidi.

Kwa kuwekeza katika uwezeshaji wa Wanawake, nina imani Taifa linajenga msingi thabiti wa usalama wa chakula na uchumi endelevu. Wanawake wakipewa nafasi sawa na wanaume katika kilimo cha umwagiliaji na upatikanaji wa zana bora za kilimo, watakuwa mstari wa mbele katika mapinduzi ya kilimo na maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Hongereni sana na nawatakia maadhimisho mema ya Siku ya Wanawake Duniani 2026.

Nafasi ya Wanawake katika kilimo na usalama wa chakula ni ya kipekee katika kutekeleza Dira 2050. Wanawake wanahusika moja kwa moja na kwa kiwango cha juu katika mnyororo wa thamani wa kilimo na usalama wa chakula. Wanawake wanahusika kwenye uzalishaji, uchakataji, uaandaji, uhifadhi na uuzaji wa chakula. Wanawake wamekuwa mstari wa mbele kuhakikisha familia na jamii zinapata chakula cha kutosha na chenye lishe bora (zingatia kazi mahiri za mama lishe).



Prof. Peter L. M. Msoffe
**Naibu Katibu Mkuu (Maendeleo ya Mazao na Usalama wa Chakula)**

Ni muhimu kwa watendaji Serikalini na taasisi binafsi kutekeleza na kusimamia mipango na miradi inayolenga kuwawezesha Wanawake walio ndani ya mnyororo wa thamani wa kilimo na usalama wa chakula. Uwezeshaji huu utachangia kufikia fursa za kiuchumi, kuongeza tija mashambani, na kuhakikisha familia zetu zinapata lishe bora na chakula cha kutosha. Kupitia uwezeshaji huu, Wizara ya Kilimo imeweka mazingira wezeshi kupitia miradi yake katika kutoa nafasi kwa Wanawake kutumia teknolojia za kisasa, mbegu bora, na mbinu endelevu za kilimo ili kuongeza uzalishaji.

Vilevile, uwezeshaji wa Wanawake kiuchumi unaimarisha sauti yao katika vyombo vya maamuzi vinavyohusiana na maendeleo ya Sekta ya Kilimo na usalama wa chakula. Ushiriki wa Wanawake katika uongozi wa vyama vya wakulima, vikundi vya kijamii, na vikundi vya ushirika unaleta mtazamo mpya na suluhisho endelevu kwa changamoto zinazokabili Sekta ya Kilimo.

Kuelekea Siku ya Wanawake Duniani 2026, Nawapongeza Wanawake kwa ushiriki thabiti katika maendeleo ya Kilimo na usalama wa chakula. Hakika Haki na Usawa kwa Wanawake na Wasichana ndio Msingi Jumuishi kufikia Dira 2050




PRODUCE OF
TANZANIA
Eatfresh




KILIMO NI MSINGI WA UCHUMI WA MWANAMKE
MWANAMKE NA KILIMO NI MAENDELEO
MWANAMKE NI MOYO WA UZALISHAJI.
MWANAMKE SHAMBANI NI BARAKA YA TAIFA
MWANAMKE NI NGUZO YA CHAKULA CHA FAMILIA
FARMALL





Kwa mujibu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) zaidi yaasilimia 65 ya Wanawake wanaofanya kazi nchini wanajishughulisha na kilimo, na wengi wao wakiwa ni wakulima wadogo. Ukweli huu unaonesha wazi kuwa Wanawake ni mhimili muhimu katika kuimarisha usalama wa chakula nchini.

Kupitia urasimishaji wa Sekta ya Kilimo unaoendelea, udhibiti wa biashara ya mazao, matumizi ya mifumo ya kidijitali, na uimarishaji wa viwango vya uzalishaji na biashara, COPRA inaendeleza na kuimarisha usawa wa ushiriki wa Wanawake katika kilimo-biashara kwa kuzingatia:



- Uwazi wa bei na upatikanaji wa taarifa sahihi za masoko, zinazoendana na mwelekeo wa bei za kikanda na kimataifa;
- Upatikanaji rahisi wa huduma, vibali na mifumo ya kidijitali, kwa kupunguza au kuondoa urasimu usio wa lazima na gharama zisizo za moja kwa moja;
- Ushindani wa haki katika masoko rasmi, unaopunguza mianya ya unyonyaji na kuongeza fursa sawa za kibiashara;
- Usimamizi wa tija kwa mkulima, kupitia kuhimiza matumizi ya mbegu bora na uzalishaji unaozingatia viwango, ili kuongeza uzalishaji na kipato; na
- Kufungua na kuimarisha masoko makubwa ya kitaifa na kikanda, yanayopanua wigo wa biashara na kuongeza thamani ya mazao.

Hatua hizi zinawawezesha Wanawake wakulima na wafanyabiashara kushiriki kikamilifu katika uchumi rasmi, kuongeza tija na kipato, na kuchangia ukuaji endelevu wa Sekta ya Kilimo.

COPRA itazidi kuimarisha mifumo hii ili Wanawake wakulima na wafanyabiashara washiriki kikamilifu, kwa tija na kwa manufaa ya uchumi jumuishi wa Taifa.

Hongereni Wanawake wakulima - nguzo ya maendeleo ya Tanzania.

Irene M. Mlola
**Mkurugenzi Mkuu**
**Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko (COPRA)**



Beatrice Banzi
**Mkurugenzi Mkuu**
**Bodi ya Chai Tanzania**

Napenda kutumia fursa hii kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani 2026 kwa kutambua na kuthamini mchango mkubwa wa Wanawake katika kukuza na kuendeleza Tasnia ya Chai nchini. Wanawake wamekuwa nguzo muhimu katika uzalishaji, uchakataji na biashara ya Chai, wakionesha bidii, uadilifu na ubunifu unaochangia kukuza uchumi wa familia na Taifa kwa ujumla. Kupitia juhudi zao, Tasnia ya Chai imeendelea kuwa chachu ya ajira na kipato kwa maelfu ya Watanzania.

Bodi ya Chai Tanzania inaendelea kuweka mazingira rafiki yanayowawezesha Wanawake kushiriki kikamilifu katika mnyororo mzima wa thamani wa zao la Chai ikiwemo upatikanaji wa miche bora, mafunzo ya kitaalamu na masoko yenye tija. Tunaamini kuwa uwezeshaji wa mwanamke ni uwekezaji wa moja kwa moja katika ustawi wa jamii na maendeleo endelevu ya Sekta ya Kilimo.

Aidha tunamuunga mkono wa dhati Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa juhudi zake za kuhamasisha usawa wa kijinsia na kuwainua Wanawake katika nafasi za maamuzi na uongozi. Maono yake yameendelea kufungua milango ya fursa kwa Wanawake katika sekta mbalimbali ikiwemo kilimo na biashara ya mazao ya kimkakati kama Chai. Kwa pamoja tutaendelea kujenga Tasnia ya Chai imara, jumuishi na yenye ushindani ndani na nje ya nchi.





Katika kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani, nawapongeza wanawake wote kwa mchango wao mkubwa katika maendeleo ya jamii na taifa.

Kupitia Mfuko wa Udhamini wa Pembejeo za Kilimo (AGITF), tunaendelea kuunga mkono uwezeshaji wa wanawake ili kuhakikisha wanapata fursa sawa za kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi.

Heri ya Siku ya Wanawake Duniani.

Mwanahiba M. Mzee
**Mkurugenzi Mtendaji**
**Mfuko wa Udhamini wa Pembejeo za Kilimo (AGITF)**

Wanawake wanapopewa nafasi ya Kutunga na kusimamia utekelezaji wa Sera, Taifa huwa na Dira; Wanapoongoza Mageuzi ya ki uchumi, Jamii hupata Nguvu; na wanapoendelea kutimiza wajibu wao kama Mama Jamii huhuishwa na kuneemeka. Mpe nafasi Mwanamke na muwezeshe katika Uongozi nawe utakuwa umewezesha vizazi katika Ustawi, Kusudi, na Hatima.




Dkt. Yasinta Nzogela
**Mkurugenzi wa Maendeleo ya Mazao**
**Wizara ya Kilimo**

Tunaposherehekea Siku ya Wanawake Duniani, tunatambua kwa dhati kuwa mawasiliano na upatikanaji wa taarifa katika Sekta ya Kilimo ni nyenzo muhimu za kuchochea maendeleo ya Taifa. Kupitia taarifa sahihi na za wakati, wanawake wakulima wameendelea kupata maarifa ya mbinu bora za kilimo, elimu kuhusu teknolojia za kisasa, na ufahamu mpana juu ya fursa za masoko.



Hii imekuwa chachu ya kuongeza uzalishaji, kipato, na kuboresha maisha ya familia pamoja na jamii kwa ujumla.

Aidha, tunapaswa kutambua kuwa wanawake ni sauti yenye nguvu na wana nafasi ya kushiriki kikamilifu katika maamuzi, mafunzo, na upatikanaji wa taarifa, ilI kuendeleza kilimo endelevu.

Tagie Daisy M.
**Boss Lady la Mawasiliano**
**Wizara ya Kilimo**



“Mwanamke, wewe ni nguvu ya asili, wewe ni mshindi, wewe ni mwalimu! Endelea kupanda mbegu za matumaini, uvune mavuno ya mafanikio, na usikubali vikwazo viwepo kwenye njia yako ya mafanikio! Wewe ni jasiri, wewe ni hodari, na wewe ni mwenye uwezo wa kufanya makubwa!"  Raha Aloyce, **Mkurugenzi Raha Farm**








Mha. Anna Mwangamilo
**Mkurugenzi wa Zana na Kilimo na Uongezaji Thamani**
**Wizara ya Kilimo**

Tunaposherehekea Siku ya Wanawake Duniani, napenda kuwahamasisha wanawake wenzangu hasa vijana wa kike kujihusisha na kilimo kwa kutumia teknolojia bora na za kisasa ili kuongeza tija, kupunguza gharama, na kulinda mazingira.

Ni wakati wa kuikumbatia sayansi na ubunifu kutoka mbegu bora, zana bora na za kisasa, umwagiliaji wa kisasa, hadi matumizi ya simu na mitandao kufuatilia masoko. Tukitumia teknolojia, tunajenga kilimo chenye faida, kinachohimili mabadiliko ya tabianchi, na kinachowapa wanawake nafasi ya kuongoza kwa ujasiri. Wanawake, kilimo cha kisasa ni chako, ni chetu, na ndicho kitakachobadilisha kesho yetu.



Vumilia Zikankuba
**Mratibu wa Mradi wa BBT**
**Project 1**
**Wizara ya Kilimo**

**"Chukua Hekima za Wanawake kutoka pande za Dunia na Uishi nazo Daima"**

bbt
Building a Better Tomorrow





"Nawapongeza wanawake wote katika taaluma ya ukaguzi kwa mchango wao mkubwa katika kuimarisha uwajibikaji, uwazi na uadilifu.

Weledi na uthubutu wenu ni msingi wa usimamizi bora wa rasilimali na maendeleo endelevu ya taasisi zetu. Tuendelee kuwawezesha wanawake kushika nafasi za uongozi na kufanya maamuzi kwa mustakabali imara wa taifa."

Asia Mohamed
**Mkaguzi Mkuu wa Ndani**
**Wizara ya Kilimo**


“
Ushiriki wa wasichana na wanawake katika Kilimo Biashara ni nguzo muhimu ya kutekeleza Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050 kupitia uzalishaji wenye tija, ujumuishaji wa jamii, na Maendeleo Endelevu
Dkt. Adella A. Ng'atigwa
**Mkurugenzi Msaidizi**
**Sehemu ya Sera Utafiti na Ubunifu**
**Wizara ya Kilimo**

**Ni muhimu kuhakikisha kuwa Wanawake na Wasichana wanapata fursa Sawa katika Ajira na Nafasi za Uongozi, kwa kuwa wao ni nguzo na Chachu muhimu ya Maendeleo ya Kiuchumi na Kijamii.**



Neema Fedrick Kivugo,
**Mkurugenzi Msaidizi**
**Sehemu ya Rasilimaliwatu**
**Wizara ya Kilimo**

WIZARA YA KILIMO
MINISTRY OF AGRICULTURE






Horticulture for Health and Wealth

Siku ya Wanawake Duniani ni siku ya kutafakari nafasi ya mwanamke katika jamii. Katika uongozi, nafasi ya mwanamke ni fursa ya kipekee ya kuonesha kwa vitendo na kuleta mabadiliko chanya katika majukumu yangu kama Mkurugenzi Mtendaji wa **TAHA**.

Kwa takribani miaka 20, nimeongoza sekta ya horticulture nchini, nikiwa mstari wa mbele katika mageuzi ya mnyororo wa thamani, utekelezaji wa Kanuni Bora za Kilimo (GAP), utambuzi na ufunguzi wa fursa za masoko, kuimarisha mazingira ya uwekezaji, na kuhakikisha matumizi sahihi ya teknolojia rafiki kwa mazingira ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Hatua hizi zimeongeza thamani ya mauzo ya nje ya mazao ya horticulture kutoka Dola za Marekani **milioni 64** mwanzoni mwa miaka ya 2000 hadi takribani Dola **milioni 600** mwaka 2025.

Kupitia TAHA, nimepata nafasi ya kuwawezesha Wanawake kwa kutoa mafunzo ya ujasiriamali na kuimarisha nafasi zao za uongozi. Maelfu ya wakulima na wajasiriamali Wanawake wamepata fursa ya kusikika katika majadiliano ya sera na majukwaa ya kitaifa na kimataifa.



Dkt. Jacqueline Mkindi

**Mkurugenzi Mtendaji - TAHA**


HORTI
LOGISTICA
Arusha


KILIMO
groecologi al
rm product



***Haki na Usawa kwa Wanawake na Wasichana; Msingi Jumuishi kufikia Dira 2050***

Happy Paschal Kitingati
**Mkurugenzi Msaidizi wa Masoko ya Mazao ya Kilimo**
**Wizara ya Kilimo**



"

Tuwawezeshe Wanawake Na Vijana Kushiriki Katika Kilimo Kinachozingatia Uhifadhi Wa Mazingira Kwa Maendeleo Endelevu Ya Nchi Yetu.

**Zainabu Sheuya**
**Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mazingira**
**Wizara ya Kilimo**



Hadija Jabiri
**Mwanzilishi Mwenza na Mkurugenzi Mtendaji**
**GBRI Business Solutions/EATFRESH**

Najivunia kuwa mjasiriamali kijana, mwenye dhamira ya kuwaunganisha wakulima wadogo na masoko ya kimataifa yenye thamani kubwa kama mchango wangu wa kutekeleza maono ya Serikali ya kukuza Sekta ya Kilimo cha mboga mboga na matunda nchini. Kwa mfano, Kampuni yangu ya GBRI inafanya kazi na maelfu ya wakulima wadogo kwenye nchi za Tanzania, Burundi na Rwanda kwa kukusanya, kufungasha na kusafirisha mazao ya bustani, hususan parachichi.

Katika kuelekea Siku ya Wanawake Duniani 2026, nachukua fursa hii kuwapongeza wanawake wote wanaothubutu kuota, kuanzisha na kuendeleza biashara licha ya changamoto. Mwanamke anapoinuka kiuchumi, familia na jamii huinuka pamoja naye. Tuendelee kuaminiana, kuinuana na kujenga mustakabali wenye usawa na ustawi kwa vizazi vijavyo.



Nyabaganga D Taraba

**Afisa Habari Mkuu Daraja la Kwanza**

**Wizara ya Kilimo**

Wanawake wana mchango mkubwa katika maendeleo ya Sekta ya Kilimo nchini. Katika kuimarisha tija na ufanisi wa uzalishaji, ni muhimu kuwawezesha wanawake kwa kuwapatia teknolojia rafiki wanazoweza kuzimudu katika utekelezaji wa kilimo kinacho stahimili mabadiliko ya tabianchi (Climate Smart Agriculture) Hatua hii itawawezesha kutumia mbinu za kisasa katika uzalishaji na usimamizi bora wa shughuli za kilimo bila kuathiri mazingira.

Kupitia uwezeshaji huo, matokeo yake ni kuimarika kwa usalama wa chakula, kuongezeka kwa utunzaji sahihi wa mazingira pamoja na kukuza kipato cha familia na Taifa kwa ujumla. Hivyo basi, mwanamke ni mhimili muhimu katika maendeleo ya sekta ya kilimo, na anastahili kuthaminiwa na kupewa nafasi stahiki ili aendelee kutoa mchango wake kikamilifu katika maendeleo ya jamii na Taifa.

Wanawake ni Nguzo ya Maendeleo, Walezi na Viongozi wenye maono. Hivyo tusherehekee nguvu, ujasiri na mchango wa kipekee wa mwanamke katika Jamii.

Agnes Desdery Hugo
**Afisa Tawala Mkuu**
**Wizara ya Kilimo**





Wanawake ni Nguzo ya Maendeleo, Walezi na Viongozi wenye maono. Hivyo tusherehekee nguvu, ujasiri na mchango wa kipekee wa mwanamke katika Jamii.Ndani ya kila mwanamke kuna ujasiri, nguvu na chachu ya maendeleo. Kwa pamoja tunaongeza thamani ya maisha katika jamii, taifa na dunia.

Maria A. Mtui
**Meneja Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo**
**Wizara ya Kilimo**



Angela K. Anatory
**Mkurugenzi wa Huduma za Sheria**
**Wizara ya Kilimo**

Katika kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani, ninatoa pongezi za dhati kwa wanawake wote kwa mchango wao mkubwa katika familia, jamii na taifa. ninatambua mchango mkubwa wa wanawake katika kuimarisha sekta ya kilimo na usalama wa chakula. Uwezeshaji wao ni hatua muhimu kuelekea kufikia malengo ya Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050.



Mabadiliko ya kidijitali *(Digital Transformation*) katika mnyororo wa wa thamani Kilimo (agriculture value chain) ni chachu ya kuongeza chakula na kukuza pato la uchumi nchini. Wahusika mbalimbali wanaounganishwa na mtiririko wa bidhaa, fedha, taarifa na huduma zinazotokana na Mnyororo huu.

Violet Kazimoto
**Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA**
**Wizara ya Kilimo**

Mungu ametupa uwezo wa kipekee wa kufanya shughuli nyingi kwa wakati mmoja. Tutumie talanta yetu vizuri kwa manufaa ya jamii na Taifa kwa ujumla.



Joyce Ngatara
**Katibu Makhsusi wa Waziri**
**Wizara ya Kilimo**

"Wanawake kwa pamoja, tunaamini kuwa Sekta ya Kilimo iliyo jumuishi ni msingi wa uchumi imara. Maendeleo ya mwanamke mkulima ni maendeleo ya familia, jamii na Taifa kwa ujumla",

Mkejina Yusuph Mkwawa
**Mpokezi Mwandamizi**
**Wizara ya Kilimo**





Kuelekea Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, ninaamini kuwa wanawake wakipewa fursa sawa na kusimamia vizuri rasilimali walizonazo, wanaweza kuwa chachu muhimu ya maendeleo ya familia, jamii na Sekta ya Kilimo.

Hindu M. Jumaa
**Mhasibu Daraja la Kwanza**
**Wizara Kilimo**



Wanawake wahasibu ni nguzo muhimu katika kujenga maadili na usimamizi wa fedha. Wanaonyesha weledi wa Hali ya juu katika taaluma inayohitaji umakini mkubwa hivyo kuondoa Dhana potofu ya kuwa uhasibu ni uwanja wa wanaume pekee .

Acpa Latifa Abdi Tunguly
**Mhasibu Mkuu Daraja la Pili**
**Wizara ya Kilimo**

# *Haki na Usawa kwa Wanawake na Wasichana; Msingi Jumuishi kufikia Dira 2050*



Upendo Mndeme
**Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Huduma za Ugani**
**Wizara Kilimo**

Upatikanaji wa pembejeo za kilimo, ikiwemo mbegu, ni chachu muhimu katika kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo. Ni wazi kuwa ili kufikia utoshelevu wa chakula katika ngazi ya familia na Taifa kwa ujumla, mbegu inaendelea kuwa rasilimali muhimu zaidi, hususan mbegu bora.

Kwa kutambua umuhimu huo, ni dhahiri kuwa mbegu ni lishe bora, mbegu ni afya na mbegu ni shibe. Hivyo, kuelekea maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, ninaweka nguvu zaidi katika kuhakikisha mbegu pamoja na pembejeo nyingine za kilimo zinawafikia wakulima kwa wakati, hususan katika mazao ya ngano, alizeti na mpunga. Ninaamini kuwa kilimo si tu chanzo cha chakula bali pia ni kipato muhimu kwa mwanamke.



Kissa Chawe
**Mkurugenzi Msaidizi,**
**Sehemu ya Uzalishaji Mazao,**
**Idara ya Maendeleo ya Mazao**
**Wizara ya Kilimo**


Better Tomorrow
Wealth







# SIKU YA WANAWAKE DUNIANI 2026